Yale ambayo mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kufanya

8.1 Usuli 43

8.2 Mashauri kuhusu dhima ya mashirika yasiyo ya kiserikali 43

8.3 Mashauri ya mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu utendaji bora wa kazi 44

KUDONDOA MBUNI, KITABU CHA PICHA, PICHA NA. 38

8

Yale ambayo mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kufanya

Sura hii inapendekeza baadhi ya mawazo ya kutendwa na mashirika yasiyo ya kiserikali yanapofanya kazi na wakulima wadogo na wengineo ili kusaidia kutekeleza viwango vya kazi. Pia inajumuisha baadhi ya mapendekezo ya utendaji bora wa kazi kwa makampuni yanayofanya kazi na wakulima wadogo. Mapendekezo haya yametokana na tajriba za wanachama wa ETI kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali.

8.1 Usuli.

Mikakati iliyoendelezwa vyema itahitajika ili kuwezesha idadi kubwa ya wakulima wadogo wanaohusika sasa katika mitungo ya ugavi ya ulimwengu kuteleza na kudumisha mgawo wa mazao katika soko la nje. Mashirika yasiyo ya kiserikali yatahofia kwamba kuongezeka kwa udhibiti wa wakulima wadogo huenda kukawapunguzia wanaouza kwenye soko la nje gharama kwa kuchukua mazao machache kutoka kwao, jambo ambalo litasababisha athari mbaya kwa watu vijijini katika nchi zinazogawa.

8.2 Mashauri kuhusu dhima ya mashirika yasiyo ya kiserikali.

Ili mwongozo wa wakulima wadogo uwe wa kufaa, ni lazima wakulima wadogo waamini utaratibu huu na wajihisi kuwa wana mamlaka fulani katika utekelezaji wake. Ingawa baadhi ya makampuni yana uhusiano bora na wakulima wadogo, sio makampuni yote yaliyo na uhusiano wa kutamanika. Mashirika yasiyo ya kiserikali yana ukwasi wa uzoefu wa kiufundi ulio muhimu sana ambao unaweza kuyafaidi makampuni na wakulima wadogo walio tayari kuwa wenza wao kikazi. Yafuatayo yaweza kufanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika swala hili:

- Kutoa msaada wa usimamizi na wa kujenga uwezo wa wakulima wadogo na makundi ya wakulima wadogo, kuendeleza uwezo wao wa kufungamana na wateja na makampuni na pia kujenga njia za kupata majibu katika uhusiano baina ya mkulima mdogo na kampuni.
- Kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa makampuni kwa kuwasaidia waendeleze mtazamo unaomlenga mkulima zaidi, na kuongeza ubayana katika uhusiano baina ya kampuni na wakulima wadogo, kwa mfano, kwenye masuala ya bei na uamuzi wa ubora wa bidhaa;
- Kuanzisha na kusaidia ushirikiano kati ya wakulima wadogo, makampuni na watoaji mikopo au pembejeo zinginezo;
- Kuchukua nafasi kama watu wa kati baina ya wakulima wadogo na makampuni;
- Kutambua mapengo katika maarifa ya wakulima wadogo na kutoa pamoja na kutekeleza nyenzo na taratibu zinazofaa;
- Kutoa vidokezi muhimu vya mwongozo 'vitakayomsaidia mkulima' kutekeleza mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI, vikiwemo vielezo na orodha ya ukaguzi vilivyotafsiriwa kwa lugha za kienyeji inapohijtajika;
- Kufunza makampuni na wakulima wadogo mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI na kusaidia upangaji wa kutimiza masharti yake;
- Kuunda njia za kutoa habari kwa wakulima wadogo kwa misingi ya kudumu. Kwa mfano, wanaweza kufanya hivi kupitia wagawaji vijijini kama vile maduka ya vifaa vya kilimo ambako wakulima wadogo wengi hupata ushauri kuhusu pembejeo, uwekezaji na shughuli za kilimo;
- Kuendeleza uwezo wa wagawaji wa huduma za maendeleo ya kibiashara ya wenyeji ili waweze kutoa mafunzo ya kufaa kwa wakulima wadogo;

- Kuasisi njia za kusimamia, kama vile vikundi kujithibitisha na kujisaidia (sambamba na njia za mambo juu ya fedha kidogo zenye misingi ya kijamii) vinavyoendelezwa kwa uzalishaji wa mazao yasiyotumia kemikali ogani?
- Kutumia mtazamo wa kijamii wa kuwezesha kutekeleza viwango vya kazi, kwani sheria zilizotungwa na sera peke yake hazitoshi.

8.3 Mashauri ya mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu utendaji bora wa kazi

8.3.1 Ujira na bei

Mashirika yasiyo ya kiserikali yana shaka kuhusu ujira mzuri na bei za haki kwa wakulima wadogo na wafanya kazi wao. Sehemu ya tatizo hasa ni asili ya mazao. Mazao yanayoharibika upesi au yasiyoweza kuhifadhiwa kwa urahisi huenda yakahitaji mipango ya uhifadhi inayohitaji uangalifu mkubwa na gharama ya juu au kuuzwa pasi kuchelewa. Kutokana na hayo, wakulima wadogo wanapozalisha bidhaa ziharibikazo upesi wanabidika hasa kuingia katika mikataba ili kuuza mazao yao upesi. Hii itawafanya wategemee sana mapato ya bei ya wakati wanapouza bidhaa zao; hivyo basi, kusababisha kushuka sana kwa bei au kupatikana kwa bei nzuri wakati mwingine. Pamoja na hayo, haja ya kuuza upesi pia inasababisha wakulima wadogo kuwauzia walanguzi. Hawa wanaweza kuwa wawekewa rehani wa mazao ambao hulipia mapema kiwango kisichobadilika japo kiwe na ubora wa juu. Hata hivyo ni nadra kwao kutoa mapatano mazuri ya uuzaji (ingawa wakati mwingine pia wanatoa manufaa kama mikopo ya mahitaji mengineyo kwa mfano, utabibu). Sifa za mimea hutiliwa maanani wakati wakulima wanapohitaji mikopo, kiasi wanachohitaji na jinsi mkopo ulivyo muhimu kwa ukulima (yaani, kama ni lazima kwa kila mkulima kuchukua mkopo).

Mkopo, na urahisi wa kuupata, huweza kuwaweka hatarini wakulima san asana wanapobadilisha ruwaza zao za uzalishaji ili kutimiza viwango vya mitungo ya maduka makuu. Sababu zinazofanya mazao yenye kuharibika upesi kuwa muhimu kwa wakulima wadogo ndizo zinazowafanya kuwa katika mtungo wa ugavi wa mazao hayo. Mazao haya yanaelekea kuwa na hatari nyingi. Hayawezi kukuzwa katika mashamba makubwa. Mawese, mpira na nazi (kwa ajili ya mafuta) mara nyingi huzalishwa katika mashamba makubwa mno kwa kuwa mazao hayo yanaweza kukuzwa peke yao, yana hatari ndogo ya kuharibika, na yanaweza kuendelea kuzaa kwa muda mrefu (ikiwa yamepandwa vizuri). Hata hivyo, mazao yenye hatari nyingi, kama njegere, nafaka na mimea mingine ya kigeni, huzalishwa kwa wingi chini ya mifumo ya ukulima wa mkataba. Wauzaji wa rejareja na wateja mara nyingi hununua mazao haya kutoka kwa wakulima wadogo kupitia mikataba. Matokeo yake ni kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya madaraja ya mtungo na uhuru mdogo kwa wakulima wadogo wa kuuza kwa bei ya juu inayoweza kupatikana.

Kuna suluhu kadhaa kwa masuala ya bei/ujira bila kujali mimea inayokuzwa na wakulima wadogo. Wateja na wauzaji wa rejareja wanaweza kuweka bei na mzalishaji bila kujali kama kuna furiko au upungufu/uhaba wa bidhaa ambayo mara kwa mara hufanya bei kubadilikabadilika. Wateja, wauzaji wa rejareja, mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya wafanya kazi wanaweza kusaidia wazalishaji kuweka nyenzo za kuhifadhi mazao yanayoharibika upesi. Wauzaji wa rejareja na wateja wanaweza kusaidia kujenga nyenzo hiyo kama malipo ya kabla jinsi inavyofanyika kwa maagizo makubwa ya bidhaa nyingine nyingi. Huenda tendo hili likawafaidi wauzaji wa rejareja na wateja kwani watapata bidhaa zenye ubora wa hali ya juu zaidi kwa vipindi vya mara kwa mara. Wauzaji wa rejareja, mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya wafanya kazi wanapaswa kuhimiza uundaji wa vyama vya wazalishaji ili kuwawezesha wakulima kusaidiana wenyewe kwa wenyewe na kuepuka walanguzi.

8.3.2 Mapato halisi na uwezo wa kupata mkopo

Mara kwa mara hili ni suala kuu kwa wakulima wadogo ambao kwa desturi hawana uwezo wa kupata mkopo huku pia kukiwa na ucheleweshwaji wa malipo yao pamoja na kuwa na ujira wa chini. Baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali (kwa mfano, Oxfam) wamesema kwamba uwezo wa kupata mkopo (sambamba na uthabiti/kudumu kwa uhusiano ya kibiashara) angalau ni muhimu kwa wakulima wadogo kama ilivyo bei yenyewe, na wakati mwingine, hata zaidi ya bei.

Mashirika yasiyo ya kiserikali na watu wengineo wanaweza kufanya kazi na makampuni kutoa suluhisho kwa matatizo kama haya, kwa kuangalia masuala ya mapato halisi kama sehemu ya muundo wa maagizo/malipo. Kwa mfano, malipo ya mbele kwa wakulima, kama vile arbuni wakati wa kuagizia, yanaweza kusaidia kupunguza baadhi ya matatizo sugu ya mapato halisi. Aidha wateja/wauzaji wa rejareja wanaweza kutoa usaidizi wa kiufundi utakaowawezesha wakulima wadogo kushinda kikwazo cha mwanzo cha ongezeko la gharama/ujuzi unaohitajiwa katika matayarisho ya kutimiza viwango vya kazi.